JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu ;
+255 (0) 717315633
+255 (0) 678 231 534
Email. Temekesecondary@yahoo.com

Shule ya Sekondari Temeke
S.L. P 46212
Dar es Salaam.
Tarehe 31/03/2022

Mzazi/Mlezi wa;

.....

S.L.P .....

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TEMEKE HALMASHAURI YA TEMEKE MKOA WA
DAR ES SALAAM MWAKA 2022/2023

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya .....

Shule ya Sekondari Temeke ipo umbali wa Kilometa 3 Kusini Magharibi mwa Wilaya ya Temeke.

Usafiri wa basi;

- *Kutoka Mwenge unapanda gari la Temeke Mikoroshini (Shuka Maghorofani/Sokoni)*
- *Kutoka Kariakoo unapanda gari la Gongolamboto kupitia Nyerere Road (Shuka Tazara)*
- *Kutoka Ubungo unapanda gari la Tandika/Gongolamboto kupitia Mandela road (Shuka Sokoni/Tazara)*
- *Kutoka Makumbusho unapanda gari la Gongolamboto kupitia Mandela road (Shuka Tazara)*
- *Kutoka Mbagala unapanda gari la Gongolamboto, Ubungo au Buguruni (Shuka Sokoni)*

Muhula wa masomo kwa Mwaka huu utaanza tarehe ....., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni siku ya tarehe .....

Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

Edit with WPS Office

1.1. SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

I. SURUALI rangi “Dark Blue”, (isipungue inch 14-16 chini) Shati jeupe lisilobana la mikono mifupi. Tai ya rangi ya Dark Blue na mistari Myeupe.
II. Soksi nyeusi
III. Mkanda mweusi wa ngozi usio na urembo
IV. Viatu vyeusi vya ngozi, vya kamba visivyochongoka mbele, visivyo na urembo wala kisigino kirefu.
V. Fulana (fulana zenye kola) zinapatikana hapa Shuleni.
VI. Nguo za michezo (Track suit dark blue)
VII. Sweta rangi ya (dark blue) lenye mshono wa (V) mbele.
(kwa watakaohitaji zitapatikana shuleni)

B. WASICHANA

I. SKETI ndefu zinazovuka magoti mshono wa (linda boksi moja kubwa) rangi “Dark Blue”.
Shati jeupe lisilobana la mikono mifupi, Soksi nyeupe na Tai ya Dark blue na mistari myeupe.
II. Wanaovaa hijabu lazima wavae nusu kanzu.
III. viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyochongoka mbele, visivyo na urembo wala kisigino kirefu.
IV. Fulana (wote) “fulana zenye kola” zinapatikana hapa Shuleni.
V. Nguo za michezo (Track suit dark blue)
VIII. Sweta rangi ya (dark blue) lenye mshono wa (V) mbele.
(kwa watakaohitaji zitapatikana shuleni)

NB. Wasichana wataruhusiwa kusuka nywele zisizopungua tano wala kuzidi saba.

1.2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

❖ *Michango inayotakiwa kulipwa na kila Mzazi/Mlezi*

NA.	AINA YA MCHANGO	KIASI CHA FEDHA (Tshs.)
1.	Ada	20,000.00
2.	Taaluma	20,000.00
3.	Tahadhari	5,000.00
4.	Ulinzi/Mazingira/Projects	20,000.00
5.	Huduma ya kwanza	5,000.00
6.	Kitambulisho na Picha	8,000.00
7.	Mitihani ya Mock	20,000.00
8.	Matengenezo/Ukarabati	7,000.00
9.	Nembo	3,000.00
Jumla		**108,000.00**

Fedha zote hizi zilipwe kupitia akaunti ya Shule, yenye Namba **A/C 20701200102 NMB** Tawi lolote. Jina la Akaunti TEMEKE SECONDARY SCHOOL, baada ya malipo u ziwasilishwe Shuleni.

Edit with WPS Office

1.3. VIFAA VIFUATAVYO VILETWE SHULENI

a) Ream 1 ya A4, na Flat file kwa ajili ya kutunzia taarifa za mwanafunzi na kopi ya matokeo (result slip).
b) Cheti cha kuzaliwa

c) VIFAA VYA USAFI

NA.	AINA YA KIFAA	IDADI	MWANAFUNZI ATALETA KIFAA (KILICHOWEKWA TIKI)
1.	Slasher	1	
2.	Mopper na mopping basin	1	
3.	Ndoo ndogo	1	
4.	Fagio la chelewa la nje	2	
5.	Fagio laini la kisasa la ndani imara la Tshs. 5,000/=	1	
6.	Mkasi wa kukatia maua size kubwa	1	
7.	Jembe na mpini wake	1	
8.	Squeezer (kisukuma maji)	1	
9.	Chepe	1	
10.	Dawa ya kudekia chooni lita 5 aina hizi: Super Gold, Tamo au Lit Pine.	2	
11.	Mfagio wa brush wa chooni	1	
12.	Reki	1	

1.4. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

- Madftari makubwa (counter book) 7 quire 4
- Mathematical set na Scientific Calculator
- Begi la Shule la mgongoni lisiwe na marembo
- Vitabu (watapewa majina na walimu wao wa masomo) Mf. somo la Biolojia
  - ✔ Biological science 3rd edition 2011 by D.J Tayler N.P.O
  - ✔ Green and G.W. Staut
  - ✔ Guide to dissection by HGQ Rowett, M.A an M.I Biology
  - ✔ Dissection kit
- Kamusi (Dictionary)
- Graph pads
- Four figures (mathematical table)

2.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni:-

Edit with WPS Office

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.

(c) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika Shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.

(f) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote; na

(h) Kutunza mali ya umma.

2.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.

i. Wizi

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote yule.

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika; Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wawapo Shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi unaokubalika na uongozi wa Shule. *Nb.* (Wasichana pekee wanaruhusiwa kusuka)

vii. Kufuga ndevu.

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

ix. Uvutaji wa sigara.

x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yote yanayovunja sheria za Nchi.

xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule.

Edit with WPS Office

xvi. Kudharau bendera ya Taifa.

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama vile; kunywa sumu *n.k*

xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

3.0. Viambatanisho na fomu muhimu virudishwe Shuleni baada ya kujaza kikamilifu.

(a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

➤ Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB. Shule hii, si ya bweni wala haina Hosteli. Hivyo, Uongozi wa Shule unawaomba wazazi na walezi kutopangisha watoto wao kwenye nyumba zilizo jirani na Shule (Hosteli Bubu).

Karibu sana Temeke sekondari

.....
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TEMEKE

KIAMBATANISHO 'B'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI TEMEKE

SIMU NA. +255 (0) 717 315 633
+255 (0) 678 231 534
KUMB NA.....

S.L. P 46212
DAR ES SALAAM
TAREHE .....

YAH : <u>FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)</u>

SEHEMU A: IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE

1. Jina la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Uraia..... dini..... dhehebu.....
4. Shule ya sekondari uliyosoma.....

PICHA YA MWANA FUNZI

Edit with WPS Office

Namba ya mtihani S. .....

5. Shule ya sekondari uliyopangiwa (FI – FIV) .....
6. Shule ya sekondari uliyotoka (FIV) namba ya mtihani S.....
7. Mahali unapoishi kwa sasa .....

Saini ya mwanafunzi..... tarehe.....

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI

1. Jina kamili la mzazi.....
2. Kazi .....
3. Anuani .....
4. Simu namba. .....
5. Sehemu unapoishi. .....

PICHA YA MZAZI

SEHEMU C: IJAZWE NA MLEZI/NDUGU WA KARIBU

6. Jina kamili la mlezi/ndugu .....
7. Kazi .....
8. Anuani .....
9. Simu namba. .....
10. Sehemu unapoishi. .....

PICHA YA MLEZI/ NDUGU

Edit with WPS Office

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI TEMEKE

SIMU NA. +255 (0) 717 315 633
+255 (0) 678 231 534
KUMB NA.....

S.L. P 46212,
DAR ES SALAAM.
TAREHE .....

YAH : <u>FOMU YA AHADI YA MZAZI KULIPA KARO NA MICHANGO YA SHULE (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI).</u>

Mimi .....
Mzazi/mlezi wa ..... wa kidato cha Tano **Mwaka 2021/2022** katika Shule ya Sekondari Temeke, nathibitisha na kuahidi kuwa nipo tayari kulipa karo ya **Tsh. 20,000/=** kwa mwaka, pamoja na michango mingine inayoidhinishwa na Shule au Mamlaka ya elimu kwa ajili ya maendeleo ya Shule na wanafunzi.

Pia, naahidi kuwa kila ifikapo mwisho wa muhula wa Shule nitakuwa nimemaliza deni kwa mwaka huo. Karo/michango utalipwa na ndugu .....
wa S.L.P ..... na simu na .....

Saini ya Mzazi/Mlezi .....
Tarehe .....

Edit with WPS Office

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TEMEKE SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
To be filled by Government Medical officer and return to the
HEAD OF SCHOOL Temeke secondary school P.O. Box 46212,

A: **RE: .....**

Please examine above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below. Say Yes or No if student has health problem and if yes then STATE.

Head mistress
Insert ✓ in the boxes provided

i.	Hearing	Yes	☐	No	☐		
ii.	Speech	Yes	☐	No	☐		
iii.	Sight	Yes	☐	No	☐		
iv.	Ts	Yes	☐	No	☐		
v.	B.P	Yes	☐	No	☐		
vi.	Diabetes	Yes	☐	No	☐		
vii.	Mental Case	Yes	☐	No	☐		
viii.	Physical Disability	Yes	☐	No	☐		

ix. Any other.....
.....
.....
.....

B: Recommend if the student is fit for studentship;
.....
.....

C: Any other advice.....
.....

Name.....
Signature.....
Date.....

Edit with WPS Office